

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 26 2322761-5  
Fax No. +255 26 2324218  
E-mail: [cna@bunge.go.tz](mailto:cna@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
10 Barabara ya Morogoro,  
S. L. P. 941,  
40490 Tambukareli,  
**DODOMA.**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU  
MKUTANO WA PILI WA BUNGE LA KUMI NA TATU (13)**

Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Tatu (13) unatarajiwa kuanza Siku ya Jumanne tarehe 27 Januari, 2026 Jijini Dodoma na kuahirishwa Siku ya Ijumaa tarehe 6 Februari, 2026.

Shughuli zitakazofanyika katika Mkutano huo ni pamoja na:-

**a) Kiapo cha uaminifu**

Kutakuwa na kiapo cha uaminifu na ahadi ya uzalendo kwa Wabunge wateule ambao hawakupata fursa ya kuapishwa katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge.

**b) Maswali**

Kama ilivyo ada katika kila Mkutano wa Bunge kunakuwa na kipindi cha Maswali Bungeni kila siku ambapo jumla ya maswali 160 yataulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Mawaziri. Aidha, kutakuwa na kipindi cha Maswali ya Papo kwa Papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu siku ya Alhamisi ambapo takriban maswali kumi na sita (16) yataulizwa na Waheshimiwa Wabunge.

**c) Hoja za Serikali**

Katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge watajadili Hotuba ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoitoa wakati akifungua Bunge la Kumi na Tatu ambayo ilieleza muelekeo wa Serikali yake.

**d) Kamati ya Mipango**

Vilevile Bunge litakaa kama Kamati ya Mipango kujadili Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/2027 – 2050/2051, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027 – 2030/2031 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**e) Uchaguzi**

Katika Mkutano huu wa Bunge, Waheshimiwa watafanya uchaguzi wa Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge pamoja na wawakilishi wa vyama mbalimbali vya Kibunge.

Ratiba ya shughuli zote zitakazofanyika katika Mkutano wa Pili wa Bunge inapatikana katika tovuti ya Bunge ambayo ni [www.bunge.go.tz](http://www.bunge.go.tz)

**Imetolewa na :** Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma  
Ofisi ya Bunge  
**Dodoma**